HABARI KITAIFA

USAFIRI

# Mwendokasi kurejeshwa kesho Mbagala kwa muda maalumu

Na Maulid Mmbaga

HUDUMA za usafiri wa Mwendokasi katika Barabara ya Mbagala kuelekea katikati ya Jiji zinatarajiwa kurejea kesho, baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila kutoa agizo.

Chalamila alitoa agizo hilo jana kwa kampuni za Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (UDART) pamoja na taasisi mbalimbali za serikali zilizo chini ya Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa alipofanya ziara ya ukaguzi.

Chalamila alifanya ziara ya ukaguzi wa vituo vya mabasi ya Mwendokasi katika njia ya Mbagala pamoja na kukagua miundombinu iliyoharibika kutokana na vurugu zilizotokea wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani Oktoba 29, mwaka huu.

Chalamila alisema watu wanaweza kujazwa maneno yenye chuki, wakawa na hasira nyingi lakini mwisho wa siku adhabu ya kinachofanyika inaweza kuwarudia wenyewe.

"Nimeona pia wananchi wa kule Kimara wanavyotaabika, Mwendokasi hakuna na mimi nimeridhia kuanzia Novemba 20 mwaka huu, saa 12 jioni hadi saa 2:00 usiku mabasi haya yawe katika barabara hii kupakia Watanzania," alisema Chalamila.

Alisema vituo vilivyoharibiwa vitawekwa utaratibu, kwamba hivi sasa serikali inaendelea kufanya tathmini ya uharibifu wa miundombinu ya umma na mali za watu binafsi, sambamba na kutambua walioathirika kiafya au kupoteza mali.

**"Nimeona pia wananchi wa kule Kimara wanavyotaabika, Mwendokasi hakuna na mimi nimeridhia kuanzia Novemba 20 mwaka huu, saa 12 jioni hadi saa 2:00 usiku mabasi haya yawe katika barabara hii kupakia Watanzania,"**

Kuhusu njia ya Mwendokasi inayotoka Gerezani kwenda Kimara, alisema serikali inaharakisha urejeshaji huduma ili usafiri urudi katika hali ya kawaida na haraka.

Aidha, alieleza kuwa migogoro ya kisiasa inaweza kuwa kati ya Watanzania lakini inawezekana yupo adui mkubwa wa maendeleo amekaa pembeni anawaangalia ili apite katikati.

"Mwisho wa siku mtajikuta mgogoro mdogo tulionao tunakaribisha majambazi wakubwa wa kiulimwengu kuja kunyang'anya kilichopo na kurudi utumwani kwenye taifa letu. Congo ilianza hivyo.

"Niwaombe sana ndugu zangu mmeona wenyewe, kwa kile ambacho mnadhani tunapaswa kukaa na kuzungumza sisi kama serikali yapo tunajifunza kutoka kwenu na ninyi inawezekana mna ushauri pia wa kutufunza ili mambo yaende sawa, kwa sababu watoto wanatakiwa kwenda shuleni, shule zikichomwa watasoma wapi?," alihoji Chalamila.

Alisisitiza kwamba watu wanapaswa kutambua kuwa miundombinu inayowekwa inawafaa wao na kizazi kijacho, hivyo ni jukumu la kila Mtanzania kuilinda.

Alisema Serikali ya Mkoa wa Dar es Salaam itafanyia kazi mambo yote yaliyotokea yakiwamo maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kukaa na kuzungumza na wananchi, ili kuendelea kuijenga Tanzania yenye umoja.

Chalamila alisema: "Lazima tukae tukubaliane, turidhiane tujenge Tanzania moja, yale mliyonayo tutayapokea na tuliyonayo mtayapokea, na kuanzia Novemba 20 magari binafsi, pikipiki na bajaji zinazopita katika njia hizi za Mwendokasi ziache kwa sababu magari ya Mwendokasi yataanza kazi."



Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam, Albert Chalamila akizungumza alipofanya ziara ya kukagua athari zilizotokea siku ya Uchaguzi Mkuu, eneo la Mbagala, Dar es Salaam jana. PICHA IMANI NATHANIEL

CamScanner

The Guardian November Jumatano 19,2025 Pg 1



Dar es Salaam regional commissioner Albert Chalamila pictured at Mbagala yesterday making remarks during a tour he used to assess the damage due to the recent (General election time) street violence witnessed in Mbagala suburb. Photo: Correspondent Imani Nathaniel

CS CamScanner

# Mwendokasi Mbagala kuanza 'ruti' kesho

Na CHRISTOPHER LISSA

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ameelekeza taasisi zote zinazohusika na Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, kuhakikisha mabasi hayo yanaanza kutoa huduma kuanzia kesho na kuvitaka vyombo vya ulinzi na usalama kuimarisha ulinzi.

Ameagiza mabasi hayo kuanza kutoa tena huduma kati ya Mbagala na Kariakoo (BRT-2) huku ukarabati wa mradi huo upande wa Kimara na Kariakoo (BRT-1), ukiendelea.

Chalamila alieleza hayo jijini Dar es Salaam, jana alipokagua miundombinu ya mradi huo iliyoharibiwa Oktoba 29, mwaka huu.

**MBAGALA-GEREZANI**

Alielekeza Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na taasisi nyingine zinazohusika na mradi huo, kuanza kutoa huduma rasmi kesho kuanzia saa 2 asubuhi.

"Itakuwa ni siku ya Alhamisi, saa mbili asubuhi nataka kuona mabasi yote njia hii ya Mbagala yanapakia abiria na kuingia barabarani,"alisema.

Alivishukuru vyombo vya dola kwa kulinda miundombinu hiyo, kwani ilikuwa katika hatari ya kuteketezwa.

"Sisi wote, Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi Tanzania, tulipiga kambi hapa Mbagala. Kama isingekuwa hivyo mabasi yote yangechomwa moto. Kama tungezembea yangekuwa ni majuto makubwa," alisema.

Alisema katika vurugu zilizotokea Oktoba 29, mwaka huu, miundombinu mingi hususan ya mradi huo na mabasi iliharibiwa.

"Nimeona namna Watanzania wa Mbagala wanavyotaabika na Mkuu wa Wilaya ya Temeke (Sixtus Mapunda) ameomba mabasi yaanze kutoa huduma,"alisema.

**GEREZANI-KIMARA**

Chalamila alisema upande wa BRT-1 inayoanzia Gerezani-Kimara, ambayo miundombinu yake iliharibiwa katika vurugu hizo, serikali inaendelea kuikarabati.

"Kwa upande wa Gerezani-Kimara, tunaharakisha kuhakikisha tunaanza kutoa huduma. Tuko katika matengenezo na tumeagiza baadhi ya vifaa vitakapofika tutaanza kutoa rasmi huduma," alisema.

**KUHUSU TATHMINI**

Chalamila alibainisha serikali inaendelea kufanya tathmini kuhusu kiwango cha uharibifu wa miundombinu ya serikali na binafsi iliyoharibiwa katika vurugu hizo.

"Pia, tunafanya tathmini ya madhara katika maisha na mambo mengine. Ninawasihi wananchi wawe watulivu, kujenga upendo na kuwa wamoja," alisema.

**ULINZI MKALI**

Mkuu huyo wa mkoa alivielekeza vyombo vya ulinzi na usalama kuimarisha ulinzi katika miundombinu na mabasi hayo.

Aidha, Chalamila alisema wananchi wa Dar es Salaam wamebeba dhamana ya maisha ya Watanzania wengi na ndani na nje ya nchi hususan nchi jirani za Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Malawi zinazotegemea Bandari ya Dar es Salaam.

"Baada ya 'lockdown' (watu kukaa ndani), kuna hasara siyo kwa fedha, bali maisha na maendeleo. Kama hali hii itajirudia madhara yake yanaweza kuwa makubwa au taifa letu litakwama kimaendeleo," alibainisha Chalamila.


**AMPONGEZA RAIS SAMIA**

Chalamila alimpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kushika tena madaraka awamu ya pili, kuunda serikali na kuendelea kujenga Tanzania yenye maelewano.

Aliwaomba wananchi kumpa ushirikiano Rais Samia kutimiza masuala aliyoahidi kuyatekeleza ndani ya siku 100.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda alimuomba Chalamila kurejesha huduma za usafiri mabasi ya mwendokasi, kwani wananchi wengi wameathirika baada ya usafiri huo kusitishwa kufuatia uharibifu wa miundombinu ulitokea Oktoba 29, mwaka huu.

## UKAGUZI



MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, akizungumza na watendaji wa taasisi mbalimbali, baada ya kukagua miundombinu ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) Mbagala, Dar es Salaam, jana. (Na Mpigapicha Wetu).

CamScanner